JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MVOMERO

SHULE YA SEKONDARI SUNGAJI
S.L.P 63,
TURIANI.

Mobile: +255 736 122 317
Email: sungajisec18@gmail.com

EDUCATION BRINGS CHANGES

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi;

……..

S.L.P …….

……..

YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SUNGAJI WILAYA YA MVOMERO KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021</u>

1.0 UTANGULIZI

Ninafuraha kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari Sungaji mwaka **2021.**

Shule ya Sekondari Sungaji ipo katika Kata ya Sungaji, Tarafa ya Turiani, Wilaya ya Mvomero; umbali wa **Km 80** Kusini mwa Mji wa Morogoro.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **11/01/2021**, Kidato cha Kwanza wote wataripoti **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **18/01/2021** (siku saba baada ya tarehe 11/01/2021)

NB: Hii ni shule ya kutwa na ya mchanganyiko

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

i) Wavulana

- ❖ Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (Tetron)
- ❖ Soksi nyeupe
- ❖ Suruali mbili za rangi ya kijivu
- ❖ Viatu vyeusi vyenye kamba (vya kupiga kiwi)
- ❖ Mkanda wa ngozi mweusi (usiwe mpana)
- ❖ Sweta lifanane na rangi ya suruali.

ii) Wasichana

- ❖ Mashati mawili meupe ya mikono mifupi (Tetron)
- ❖ Sketi mbili rangi ya kijivu ziwe ndefu kupita magoti (za heshima)
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba jozi mbili
- ❖ Sweta lifanane na rangi ya sketi.

NB: Wanafunzi wa Kiislamu wanaweza kushona (Wasichana)

- ✓ Suruali pana na ndefu pamoja na Jarabibi pana na refu, urefu wa inchi sita kutoka vifundo vya miguu na lenye mikono mirefu.
- ✓ Nusu kanzu nyeupe za mikono mirefu na Jarabibi pana na refu kufika magotini pamoja na sketi ndefu kufikia vifundo vya miguu.

2.2 NGUO ZA MICHEZO

i) Wavulana

- ❖ Bukta ya rangi ya **Blue au Trakisuti ya blue**
- ❖ Raba ya michezo rangi yoyote
- ❖ Fulana ya **Blue**

ii) Wasichana

- ❖ **Trakisuti ya rangi ya Blue**
- ❖ Raba ya michezo rangi yoyote
- ❖ Fulana ya **Blue**

3.0 VIFAA VYA DARASANI

- Daftari (Kaunta 10)
- Kalamu za wino wa bluu/mweusi – mbili
- Mkebe wa Hisabati

4.0 MAHITAJI MENGINE

- Nauli ya kwenda na kurudi ni jukumu la mzazi kwa mwanafunzi wanaotoka mbali
- Wanafunzi wanatotka mbali wanashauriwa kupanga vyumba katika vijiji vya Mbogo/Kigugu
- Shule ipo karibu na Hospitali ya Chazi, unashauriwa kukata mapema Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu ya mwanao anapougua ghafla akiwa shuleni

5.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivvorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

i) Heshima kwa walimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii) Mahudhrio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
iii) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
iv) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
v) Kutunza mazingira ya shule; usafi wa mwili na mavazi.
vi) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
vii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
viii) Kutunza mali za umma.

6.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

i) Wizi.

ii) Kutohudhuria masomo siku 90 au zaidi mfululizo bila taarifa / utoro.

iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.

v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwanafunzi mwenzako, Kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

vi) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile: Bangi, Cocaine, Mirungi, Kubeli.

vii) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.

viii) Kupata ujauzito au kutoa ujauzito.

ix) Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

x) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.

xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

xii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

xiii) Kudharau bendera ya Taifa.

xiv) Kufanya jaribio la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

xv) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

7.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

i) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

ii) Fomu ya maelezeo binafsi kuhusu histroria ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

iii) Fomu ya mzazi/mlezi kukubaliana na sheria, kanuni maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

iv) Fomu ya Taarifa za Mwanafunzi na Mzazi au Mlezi

v) Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA, SHULE YA SEKONDARI SUNGAJI

THE HEADMASTER
SUNGAJI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 63
TURIANI-MOROGORO

MKUU WA SHULE

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA AHADI

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI SUNGAJI S.L.P 63,

TURIANI

KWA MWANAFUNZI.

Mimi…….. ninakubali nafasi niiyopewa kuingia Kidato cha……..…… mwaka……. Katika shule ya Sekondari Sungaji.

Naahidi kwamba: 1. Nitatii sheria zote za shule kama nilivyozisoma 2. Nitafanya bidii katika masomo na shughuli zote za shule. 3. Nitakuwa mwanafunzi mwenye nidhamu ya hali ya juu, mkakamavu na mwenye mwenendo safi wakati wote hata nikiwa nje ya shule kwa madhumuni ya kuipa na kutunza sifa ya shule ya Sekondari Sungaji.

MUNGU NISAIDIE:

Sahihi ya mwanafunzi…….. Tarehe……

KWA MZAZI/MLEZI:

Mimi (Jina la Mzazi/Mlezi)……...

Mzazi/Mlezi wa……

Naahidi kwamba: 1. Nitampatia mwanangu mahitaji ya shule kama yalivyotajwa katika maelekezo ya kujiunga na shule 2. Nitakuwa tayari kutoa msaada wowote utakaohitajika (maoni, adhabu) katika kumlea mwanangu 3. Nitamhimiza mwanangu kufanya mazoezi yake ya masomo nyumbani (homework) na kufuatilia maendeleo yake na tabia yake shuleni. 4. Mwanangu akiwa nyumbani nitamtunza na kumwangalia vizuri mwenendo wake. 5. Nitashirikiana na walimu kumweleza mwanangu maana ya shule na umuhimu wa kuwepo shuleni.

Sain ya Mzazi/Mlezi…… Tarehe……

STUDENT'S DETAILS/ TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Student's Full Name/ Jina kamili la Mwanafunzi

Students' Birth Certificate Number (Entry No.)/ Namba ya Cheti cha Kuzaliwa cha Mwanafunzi

Other Information/ Taarifa nyingine za Mwanafunzi

Citizenship/Uraia

Health status/ Hali ya Afya

Disabilities/ Hali ya Uleamavu

GUARDIAN DETAILS/ TAARIFA ZA MLEZI/MZAZI

Guardian/ Parent's National Id Number/ Namba ya Nida ya Mzazi/ Mlezi

Full Name/ Jina Kamili

Sex/Jinsi

Relationship/ Uhusiano

Email/ Barua pepe

Phone No/ Namba ya simu

Occupation/ Kazi

Address/Anuani

Physical Address/Mahali

Educational Level/ Kiwango cha Elimu cha Mzazi/ Mlezi

Place of Domicile/ Makazi ya Kudumu ya Mzazi/ Mlezi

Region/ Mkoa

District/ Wilaya

Village/Street–Kijiji/ Mtaa

Parenting Status/ Hali ya Uyatima (**Weka × kama hapana na √ kama ndiyo**)

Baba amefariki

Mama amefariki

Baba na Mama wamefariki

MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by Medical Officer (MO) in respect of Form One Entrant

Student's name: ……..…….

Age ……..

Blood count (Red and White) ……..

Stool Examination ……

Syphilis	Test……..
T.B	Test……..
Eye	Test……..
Ears	Test…….
Chest	Test…….
Spleen	Test…….
Abdomen	Test…….

Additional information: e.g Physical defects of impairment, infections chronic or Family disease etc.

……

……

…….

I certify that the above nominee is fit/unfit for admission into day/boarding Secondary School.

Signature ……

Designation ……

Station ……

Date ……...